

# Kuishi Maisha ya Kikristo



**Kitabu hiki kinamilikiwa na:**

---

# **KUISHI MAISHA YA KIKRISTO**

Kozi Kwa Waumini Wachanga

(Waliopendekezwa ni miaka 8 - miaka 12)

Imeandikwa na Mary Lou Canata  
Imetafsiriwa kwa Kiswahili na Tegemea Mbise  
Imehaririwa na Stacy Collins  
Michoro zimetengenzwa na Eric Jansen

Imechapishwa na  
Mizizi Mobile Missions Press pamoja na  
Foursquare Missions Press  
Copyright © 2003

## **YALIYOMO**

### **Somo la Kwanza**

Mimi ni Mkristo! Sasa Iweje? **6**  
*(Kukua Katika Familia ya Mungu)*

### **Somo la Pili**

Ishi Kwa Ajili Ya Yesu **11**  
*(Maisha ya Kikristo ya Kila Siku)*

### **Somo la Tatu**

Kusoma Kuhusu Yesu **15**  
*(Usomaji wa Biblia na Kujifunza)*

### **Somo La Nne**

Kuongea Na Mungu Na Yesu **19**  
*(Maisha ya Maombi)*

### **Somo la Tano**

Kwenda Kanisani **23**  
*(Maisha Kanisani)*

### **Somo la Sita**

Kuwaambia Wengine Kuhusu Yesu **28**  
*(Kushuhudia Wengine / Uinjilisti)*

## **KARIBU KATIKA FAMILIA YA MUNGU**



Je! Si jambo la kufurahisha kujua kuwa wewe ni mali ya familia kubwa ya Kikristo ya Mungu? Wewe ni mshiriki wa familia yake na unaweza kuwa mshiriki wakati unamwamini Yesu kama Mwokozi wako, utii Neno Lake na utumie wakati kumjua vizuri zaidi.

Familia ya Mungu imeundwa na watoto wa kiume na wakike, vijana wadogo na watu wazima. Sisi ni kaka na dada. Mungu ndiye Baba yetu wa Mbinguni.


Kumwomba Mungu akusamehe kwa makosa yako inamaanisha kwamba dhambi zako za kale zinasamehewa na kusahaulika. Msamaha uliwezekana na unawezekana kwa sababu Yesu alikufa msalabani kwa ajili yako.

Kama mshiriki wa familia ya Mungu na kama Mkristo, Mungu anatarajia uishi maisha yanayompendeza. Kwa msaada wake, unaweza kuishi maisha hayo nyumbani, shuleni, kanisani, kwenye michezo - kila mahali.

Kitabu hiki kinakusaidia kujua tu yale ambayo Mungu anataka uyajue. Kwanza kuwa wewe ni mshiriki katika familia yake, pia utajua namna ya kumpendeza na kumtumikia Yesu Kristo, Mwokozi wako na Rafiki. Utakua Mkristo hodari.

### **Jifunze Mstari Huu wa Biblia:**

"Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu." Luka 2:52



Chora Picha Yako Mweyewe Katika Sanduku Hili!


Mimi, \_\_\_\_\_, Nimempokea  
Bwana Yesu Kristo kuwa Mwokozi wa maisha yangu  
\_\_\_\_\_ (taja tarehe)  
katika \_\_\_\_\_ (taja mahali).

Jina la mtu ambaye aliomba nami.

\_\_\_\_\_

Kabla ya kuanza...

Tafuta Biblia



Tafuta penseli na kifutio

Tafuta kamusi.






### ***Jinsi ya kutumia kitabu hiki...***

1. Tumia kitabu hiki pamoja na Biblia yako. Maandiko yametolewa kutoka Biblia ya Union Version.
2. Mwombe Mungu akusaidie ufanye kwa bidii.
3. Uende polepole. Soma kila somo kwanza, halafu fanya mazoezi.
4. Soma kila swali na uandike jibu.
5. Jifunze na ujue mistari ya Biblia iliyotolewa katika kila somo.
6. Kitabu kitakapokamilika, mpe mwalimu wako. Utarudishiwa kitabu chako.
7. Tunza kitabu chako kwa kusoma katika wakati ujao na kufanya marudio.
8. Washirikishe marafiki zako kitabu chako kilichokamilika.
9. Endelea kusoma Biblia yako, omba na uishi kwa Yesu.





## **Somo la Kwanza**

### **MIMI NI MKRISTO - SASA IWEJE?**

Baadhi ya watu hawana uhakika kwamba wao ni Wakristo, lakini unaweza kuwa na uhakika. Unapomwomba Mungu akusamehe mabaya uliyofanya na kumwambia Yesu unataka awe Mwokozi wako, utakuwa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ambayo ni sawa na kuwa mshiriki katika familia yake. Mungu atafanya haya kwa sababu aliahidi angefanya. Mungu hawezi kusema uongo! Soma kuhusu ahadi yake (Yohana 1:12).

Sasa kwa kuwa wewe ni wa familia ya Mungu, utataka kukua kiroho na kuwa Mkristo hodari. Hili litafanikiwa ikiwa utajifunza Neno la Mungu na kufanya kile Mungu anachokuagiza, kama mtoto wake.

Mungu hafurahishwi na tunayofanya kila wakati lakini anatupenda na atatusaidia kufanya kile ambacho kinampendeza.

"Dhambi" ni neno lingine la kutotii. Tunapotenda dhambi, bado tunaendelea kuwa washiriki katika familia ya Mungu kwa sababu Mungu huwa tayari kutusamehe wakati tunapomba msamaha wake.



Mungu anatuambia katika Biblia tunayopaswa kufanya ili kumpendeza. Tunafurahia tunapomtii Mungu, Baba yetu wa mbinguni.

Tafuta maandiko yafuatayo katika Biblia yako na uyasome na ujifunze Mungu anachotaka ufanye wewe kama mtoto wake.

1. Onyesha upendo kwa kila mtu, hata adui zako. Mathayo 5:44
2. Onyesha wema kwa kila mtu. Waefeso 4:32
3. Jifunze kusamehe wengine. Luka 6:37
4. Saidia wengine. Isaya 41:6
5. Usiibe. Kutoka 20:15
6. Usidanganye. Waebrania 13:18
7. Usiseme uongo. Mithali 12:17
8. Watii wazazi wako. Waefeso 6:1
9. Kuwa mwangalifu katika kile unachozungumza na unachofanya. Luka 6:31

Utakapofika mbinguni hautalazimika kujaribu kuwa mwema. Mbinguni, hakuna jaribu wala hakuna dhambi. Kila kitu na kila mtu atakuwa kamili. Utaishi na Mungu na familia yake milele.

## **ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?**

1. **Unajuaje kwa hakika kuwa wewe ni Mkristo?**

---

---

---

**2. Nakili mstari wa Biblia inayopatikana katika 1 Yohana 1:9.**

---

---

---

**3. Weka mstari kwenye neno lisilo sahihi katika kila sentensi:**

*Usitii, watii wazazi wako.*

*Shirikiane, Usishirikiane na wengine.*

*Onyesha wema kwa baadhi tu ya watu, kwa kila mtu.*

*Penda, chukia adui zako.*

**4. Zungushia duara jibu sahihi.**

*Mungu alitoa Biblia ili tuifuata?*

Ndiyo          Hapana

*Je! Mungu hutuagiza kutii Biblia*

Ndiyo          Hapana

*Je, Mungu hupendezwa mara zote na tunayofanya?*

Ndiyo          Hapana

*Je! Mungu hutusamehe kwa makosa yetu?*

Ndiyo          Hapana

*Je, Mungu anataka kutusaidia ili tumtii?*

Ndiyo          Hapana

**5. Jaza jina lako katika nafasi zilizoachwa wazi.**

Kwa maana jinsi hii Mungu alimpenda \_\_\_\_\_

hata akamtoa Mwanawe pekee, ili (ikiwa) \_\_\_\_\_

amwaminiye, \_\_\_\_\_ asipotee, bali awe na

uzima wa milele. Yohana 3:16

6. **Neno lingine kwa dhambi ni:** (pigia mstari chini ya jibu sahihi)

KUTII

KUTOTII

MAKOSA

UBAYA

7. **Je, inawezekana kuishi maisha ya Kikristo popote ulipo?**

Ndiyo

Hapana

Labda

Mara Pengine

8. **YESU ni nani?** Tafuta jibu katika 1 Yohana 5:5.

\_\_\_\_\_

9. **Kwa nini Yesu Kristo alikufa Msalabani?**

Soma 1 Wakorintho 15:3.

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

10. **Unapomwasi Mungu, unapaswa kufanya nini?** Soma 1 Yohana 1:9.

T \_\_\_\_\_ dhambi zetu na Mungu

A \_\_\_\_\_ dhambi zetu.

11. **Mstari wa Biblia unaotudhibitishia kuwa tutakuwa na uzima wa milele mbinguni. Je! Unaweza kujaza maneno yaliyokosekana?** Soma 1 Yohana 5:13.

Nimewaandikia \_\_\_\_\_ mambo hayo, ili

mjue ya kuwa \_\_\_\_\_ uzima wa milele, ninyi

mnaoliamini jina la \_\_\_\_\_ wa Mungu.

## 12. Pigia mstari chini ya neno "Kristo" kwenye neno "Mkristo".

### Kariri Mistari Hii ya Biblia.

"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake." Yohana 1:12

"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Yohana 3:16

"Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko."  
1 Wakorintho 15:3

Umempokea Yesu kuwa Mwokozi wako binafsi na kuamini kuwa Yesu ni Mwana wa Mungu kwa hivyo wewe ni mmoja wa watoto wake.




## Somo la Pili

### KUISHI KWA AJILI YA YESU

Kuna njia moja tu ya kuishi na kuwa na furaha, na hiyo ni kwa kuishi kwa ajili ya Yesu.


Katika Biblia, tunaona kwamba kuna kanuni tunazopaswa kufuata ili kuishi na ili tuweze kuwa jinsi Mungu alivyopanga. Hizi ni baadhi ya kanuni ambazo tumepewa na Mungu ili maisha yetu yaweze kuwa ya amani na furaha.



Mungu kamwe hakuwahi kutudai tufanye jambo bila kuahidi kutusaidia. Pale unapofanya makosa au kuvunja moja ya sheria zake, ni muhimu kumwomba Mungu msamaha. Siku zote Mungu anakusubiri ili akusamehe.

Mungu bado anakupenda hata unapofanya makosa, lakini hapendi mambo mengine yale tunayofanya. Bado wewe ni wa Mungu.

Watu wanakutazama. Je! Ulijua hii?



Unapokuwa huna uhakika ikiwa kitu fulani ni sawa au si sawa, jiulize maswali haya:

*Je! Mimi ninafanya na kusema yale yanayompendeza Mungu?*

*Je! Ninajaribu kufikiria na kusema kama Yesu?*

*Je! Mimi nawafanyia wengine kama ninavyotaka kufanyiwa?*

*Je! Ninaonyesha fadhili na upendo kwa wengine?*

*Je! Niko tayari kusaidia?*

Kutakuwa wakati ambazo Shetani atakujaribu ili ufanye mabaya. Wakati haya yanapokutokea, ongea na Mungu na umwombe msaada wake. Kumbuka, sio dhambi kujaribiwa lakini ni dhambi kujiingiza katika majaribu na kufanya vibaya.

Ibilisi ni adui yako. Yeye ni mjanja sana. Anapenda kukudanganya ili ufanye vitu vibaya. Mungu ni mwenye nguvu kuliko Shetani. Mungu atakusaidia wakati wa matatizo. Soma 1 Yohana 4:4.



## ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?

1. Orodhesha kanuni tano ambazo tunapaswa kuishi kwazo.

---

---

---

---

---

2. Je! Mungu atatufanyia nini tunapoomba msamaha kwa dhambi zetu? Soma 1 Yohana 1:9.

---

3. Zungushia "Ndiyo" au "Hapana" kwa kila sentensi.

Watu hutazama kile tunachofanya.      NDIYO    HAPANA

Watu husikiliza tunasema nini.      NDIYO    HAPANA

Mungu anataka niwe mwenye fadhili.      NDIYO    HAPANA

4. Weka X kando ya kila sentensi ya kweli.

\_\_\_\_\_ Ninapaswa kuzungumza na Mungu katika sala kila siku.

\_\_\_\_\_ Ninapaswa kufanya kitu kizuri mara moja kwa wiki tu.

\_\_\_\_\_ Ninapaswa kulitii Neno la Mungu wakati ninajisikia kufanya hivyo.

5. Ni nani anayejaribu kutufanya tufanye vibaya?

MUNGU

SHETANI

YESU

**6. Kweli au Si Kweli** Zungushia jibu sahihi.

Mungu atakuwa msaada wangu wakati wa matatizo.

KWELI                      SI KWELI

Shetani hujaribu kunijaribu kufanya mabaya.

KWELI                      SI KWELI

Kujaribiwa ni kufanya dhambi.

KWELI                      SI KWELI

**7. Nani MWENYE NGUVU na MKUBWA kuliko Shetani?**

— — — — —

**8. Je! Mungu anaweza kutujaribu?** Soma Yakobo 1:13

\_\_\_\_\_ Ndiyo      \_\_\_\_\_ Hapana

**9. Soma na ujifunze mstari huu wa Biblia.**

"Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi."  
Yohana 13:35

**10. Nakili mstari unaopatikana katika Mathayo 28:20 ambao ni ahadi ya Mungu kwetu sisi sote.**

"Na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" Mathayo 28:20 (b)

---

---

---







## Somo la Tatu

### SOMA BIBLIA YAKO



Kama vile unahitaji kula chakula kizuri kila siku ili ukue kimwili, pia unahitaji kusoma Biblia ili ukue kiroho.

Biblia ni ujumbe wa Mungu kwa watu wanaoishi Duniani. Ni kwa watu wa kila rika. Ni kitabu kimoja kikubwa lakini kina jumla ya vitabu 66; Agano la Kale likiwa na 39 na 27 katika Agano Jipya.

Usomaji wa Biblia kila siku itakusaidia...

- kujifunza kuhusu Yesu, Mwana wa Mungu.
- kujua matarajio ya Mungu kutoka kwako.
- wakati upweke au huzuni.
- wakati unahitaji msaada wa Mungu katika kufanya maamuzi.
- kukua kama Mkristo.

Soma Biblia yako KILA SIKU. Unaweza pia kujifunza kwa kusoma vitabu vya darasa la Jumapili, karatasi zako za nyumbani na vitabu vingine vya hadithi za Biblia.

Soma Biblia yako POPOTE ULIPO; nyumbani, likizo, kanisani, darasa la Jumapili, katika chumba chako mwenyewe, kwenye matembezi; mahali popote, wakati wowote.

Soma Biblia yako kwa UANGALIFU. Wakati hauelewi kile unachosoma, mwombe Mungu akusaidie kuelewa. Unaweza pia kuzungumza na mwalimu wako wa darasa la Jumapili au mchungaji kuhusu mambo ambayo huelewi.

Soma Biblia yako KWA SAUTI NDOGO au SAUTI KUBWA. Fikiria kuhusu kile Mungu anachokuambia kupitia Neno Lake, Biblia.

Soma Biblia yako MWENYEWE au na WENGINE.

### **NI WAPI UNATAKIWA KUANZA KUSOMA?**

Chaguo ni lako. Unaweza kuanzia mwanzoni kwa kusoma kitabu cha Mwanzo au kuanza na Agano Jipya. Kitabu cha Luka katika Agano Jipya ni mahali pazuri kuanzia.



### **ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?**

- 1. Pangilia maneno haya ambayo yanaonyesha unachopaswa kufanya sasa kwa kuwa wewe ni Mkristo.**

msao

Blaibi

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

2. Orodhesha mambo mawili ambayo usomaji wa Biblia utakutendea.

---

---

3. Weka X mbele ya sentensi zilizo kweli.

\_\_\_\_\_ Ninapaswa kusoma Biblia yangu kila siku.

\_\_\_\_\_ Naweza kusoma Biblia yangu kanisani tu.

\_\_\_\_\_ Biblia ni Neno la Mungu.

4. Ni nani anayeweza kunisaidia kuelewa kile nilichosoma katika Biblia?

---

5. Soma Zaburi 119:105. Je! Neno la Mungu kwako ni nini?

Neno lako ni \_\_\_\_\_ ya miguu yangu na \_\_\_\_\_  
wa njia yangu.

6. Andika na ujifunze mistari hii kwa kumbukumbu:

"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe" Mathayo 24:35

---

---

"Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, Nisije nikakutenda dhambi" Zaburi 119:11

---

---

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu " Zaburi 119:105

---

---

7. Nyumbani kwetu kuna Biblia \_\_\_\_\_ (ngapi?).

8. Andika barua kwa Mungu kuhusu Biblia na inamaanisha nini kwako.

Mpendwa Mungu,

Saini,

---

9. Mstari ninaoupenda kwenye Biblia ni:

\_\_\_\_\_ : \_\_\_\_\_



## **Somo la Nne**

### **KUZUNGUMZA NA MUNGU NA YESU**

Kuzungumza na Mungu, Baba yako wa Mbinguni, huitwa "Sala" au "Maombi." Utataka kuzungumza na Mungu wakati wote kama vile Biblia inavyokuambia kwenye 1 Wathesalonike 5:17, "Omba bila kukoma." Tunaweza kuomba wakati wowote na mahali popote.

Siku zote Mungu yuko tayari kusikia sala zetu ikiwa zinasikika kwa sauti au kwa sauti ya kunong'ona. Mungu kamwe halali hivyo unaweza kuongea naye wakati wowote, usiku au mchana. Kamwe hana mambo mengi zaidi ambayo yatamzuia kukusikia.

Hapa kuna nyakati zilizopendekezwa za kuomba:

Kabla ya kuanza siku mpya - mwombe akusaidie.

Kabla ya mlo - mshukuru kwa chakula.

Unapoogopa - mwombe ujasiri.

Unapokuwa mpweke au mwenye huzuni - mwombe akusaidie uwe na furaha.

Wakati unapokuwa na uhitaji - mwombe na umwamini yeye anaweza kutimiza mahitaji yako.

Unapotenda dhambi - mwombe akusamehe.

Unapokuwa mgonjwa - mwombe akuponyeshe.

Unapohitaji msaada - mwombe akusaidie.  
Kabla ya kulala - mwombe ulinzi.

*Hapa kuna mambo kadhaa ya kukumbuka wakati unaomba:*

- Mshukuru kwa jambo maalum aliyokufanyia.
- Kumbuka familia yako, marafiki, kanisa, wachungaji na wamishonari.
- Mwambie Mungu kuhusu shida na mahitaji yako.
- Mwisho wa sala, sema maneno haya, "Kwa jina la Yesu."  
(Soma: Yohana 14:13-14.)

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake jinsi ya kusali. Katika Mathayo sura ya 6:9-13, Anatoa mfano wa sala-



*Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe leo riziki yetu. Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu. Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.*

Wakati mwingine utaomba na watu wengine lakini ni vizuri kuwa na muda wako binafsi na Mungu. Ongea naye kama vile unavyoongea na rafiki kando na wewe. Haya ni maombi.

Unaweza kuomba katika chumba chako mwenyewe, kwenye gari, shuleni, kanisani, mahali popote. Wakati mwingine unaweza kupiga magoti wakati mwingine unaweza tu kufunga macho yako. Kanisani, mnaweza kusimama au kukusanyika kwenye duara na kushikana mikono mnaposali.

Kumbuka, Mungu anajibu maombi. Wakati mwingine, majibu yake ni "Ndiyo," wakati mwingine ni "Hapana" na wakati mwingine ni "Subiri." Yeye siku zote hutunza ahadi zake, unaweza kuwa na uhakika wa hili. Katika Warumi 4:21, tunasoma maneno haya: "huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyahidi."

Biblia inatuambia tuombeane na tuwaombee wale ambao wanaweza kututendea vibaya.

Yakobo 5:16 "... ombeaneni ili mpate kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu na mafanikio."

Mathayo 5:44 "... Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."

### **ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?**



1. "Kuongea na Mungu" ni nini? Weka X kwenye jibu sahihi.

- \_\_\_\_\_ Kuimba
- \_\_\_\_\_ Kusali / kuomba
- \_\_\_\_\_ Kusoma

2. Je! 1 Petro 3:12 inasema nini kuhusu sala zetu?

Macho yake \_\_\_\_\_

Masikio yake \_\_\_\_\_

**3. Ni lini unapoweza kuongea na Mungu?**

---

**4. Unaweza kuongea na Mungu wapi?**

---

**5. Weka "K" kwenye sentensi ambazo ni Kweli.**

\_\_\_\_\_ Naweza kuongea na Mungu wakati wowote, mahali popote.

\_\_\_\_\_ Mungu hawezi kunisikia wakati mwingine kwa sababu ana shunghuli nyingi sana.

\_\_\_\_\_ Sipaswi kuomba na wengine.

\_\_\_\_\_ Kuungama ni kukiri kwa Mungu kosa langu.

\_\_\_\_\_ Ninapaswa kuomba wengine.

\_\_\_\_\_ Kuomba kila siku ni tabia nzuri.

**6. Soma kwa sauti kubwa kisha ukariri "Maombi ya Bwana" yanayopatikana katika Mathayo 6:9-13.**

**7. Zungushaia jibu sahihi.**

Lazima nipige magoti mara zote wakati ninapoomba.

NDIYO                      HAPANA

Kuomba ni kuongea na Mungu.

NDIYO                      HAPANA

Naweza kuongea na Mungu wakati wowote, mahali popote.

NDIYO                      HAPANA





## **Somo la Tano** **KWENDA KANISANI**

Moja kati ya mahali pengi ambapo tunaweza kujifunza kuhusu Yesu na Mungu ni kanisani. Kanisa wakati mwingine huitwa "Nyumba ya Mungu." Ni mahali ambapo watu wa umri wote huja pamoja-

1. Kumwabudu na kumtukiza Mungu.
2. Kujifunza zaidi kuhusu Mungu na Mwana wake, Yesu.
3. Kukutana na marafiki wa Kikristo.
4. Kuwa na familia ya Mungu.
5. Kuimba, kuomba na kujifunza.
6. Shiriki na wengine yale ambayo Mungu ametufanyia.
7. Kufurahia ushirika wa Kikristo.
8. Kuhudhuria darasa la shule ya Jumapili (likiwepo).
9. Kufundishwa kutoka kwenye Biblia.

Kuhudhuria shule ya Jumapili na mikutano mingine tofauti ya kanisa kila wiki itakupa njia nyingi za kanisa kila wiki itakupa njia nyingi za kujifunza zaidi kutoka kwa Biblia, Neno la Mungu.

Kuna walimu na wafanyakazi ambao watawafundisha wakati wa mikutano maalum, wakati wa likizo, vilabu vya Biblia na mikutano mingine. Kujifunza zaidi kuhusu Mungu itakusaidia kuwa Mkristo mwenye nguvu, Mkristo unayekua. Hii ndio sababu moja inayosababisha kuhudhuria kanisani wakati wote.

Jumapili kawaida ni siku ambayo watu wengi wanaenda kanisani. Lakini kuna siku zingine kwenye wiki ambazo tunaweza kuhudhuria. Kanisa lako labda litakuwa na mikutano mingine ambayo hufanyika siku zingine zaidi ya Jumapili tu.

Mungu anatuambia tuisahau kwenda kanisani. Soma Waebrania 10:25. Mungu anatuambia "wala tusiache kukusanyika pamoja."

*Kwa nini kwenda kanisani?* Hili ni swali ambalo wavulana na wasichana wakati mwingine hujiuliza. Hapa kuna sababu kadhaa za kukumbuka.

Tunaenda kanisani kwa sababu:

1. Biblia inatuambia tuungane pamoja na kumwabudu Mungu.
2. Tunakua katika kumjua Mungu vizuri kwa kusikiliza mafundisho na mahubiri.
3. Tunakutana na kuwajua marafiki wengine Wakristo.
4. Tunatakiwa kuwa na muda wa ushirika wa Kikristo.
5. Tunahitaji muda wa kuyatoa mawazo yetu yote kwa Mungu.
6. Tunataka kushiriki upendo wetu kwa ajili ya Mungu.

Kuna mambo mengi utafanya kanisani. Wakati unapojiunga na wengine, utakuwa kumwabudu Mungu pamoja katika mahali pamoja.

Hii ni orodha ya mambo nane ambayo yanaweza kufanyika kanisani kwako.



**Kuimba**



**Kutoa**



**Kujifunza**



**Kushirikiana**



**Kuomba**



**Kuabudu**



**Kuhubiri**



**Kushuhudia**

Unapoenda kanisani, chukua Biblia yako na pesa yako ya sadaka.

Kwa sababu wewe ni sehemu ya kanisa, ni muhimu kuwa na heshima na kwamba unasaidia kuliweka safi.

Utataka kuwaambia wengine kuhusu kanisa lako na kuwaalika kuhudhuria pamoja na wewe.

Kujifunza kuhusu Yesu na Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, kunaweza kuburudisha na kufurahisha. Fanya kwenda kanisani iwe tabia. Itakusaidia kuishi maisha ambayo Mungu alipanga uishi.

## ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?

1. **Kanisa ni nini?** (Weka X kwenye kila sentensi iliyo kweli.)

\_\_\_\_\_ Mahali pa kumwabudu Mungu

\_\_\_\_\_ Mahali pa kuimba na kusifu

\_\_\_\_\_ Mahali pa kujifunza zaidi kuhusu Mungu

\_\_\_\_\_ Mahali pa kucheza michezo na kukosa heshima

2. **Kamilisha mstari huu wa Biblia: Waebrania 10:25**

"Wala \_\_\_\_\_ kukusanyika  
\_\_\_\_\_ kama..."

3. **Zungushia jibu sahihi.**

Je! Ninapaswa kuhudhuria kanisa lolote?

NDIYO                  HAPANA

Je! Ninapaswa kuhudhuria kanisani kila wiki?

NDIYO                  HAPANA

Je! Ninapaswa kuwaalika wengine kuhudhuria?

NDIYO                  HAPANA

4. **Ni mahali gani pazuri pa kukutana na marafiki wapya?**

\_\_\_\_\_

5. **Orodhesha vitu nane (8) ambavyo vinaweza kufanyika kanisani.**

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_



6. Taja vitu viwili unavyopaswa kuvichukua kanisani.

\_\_\_\_\_

7. Je! Unajisikiaje baada ya kwenda kanisani?

\_\_\_\_\_

8. Taja jina la kanisa unalohudhuria:

\_\_\_\_\_

9. Jina la mchungaji wako ni nani?

\_\_\_\_\_

10. Taja baadhi ya shughuli zinazofanyika kanisani kwako:

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_

\_\_\_\_\_



Naweza kusaidia kanisa kwa:

Kusaidia \_\_\_\_\_ safi.



Kuwaambia \_\_\_\_\_ kuhusu kanisa.

Kuwaalika wengine \_\_\_\_\_.

Jifunze mistari hii ya Biblia:



"Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo." Warumi 10:17

"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Mathayo 6:33





## **Somo la Sita**

### **KUWAAMBIA WENGI KUHUSU YESU**

Sasa kwa kuwa wewe ni mtoto wa Mungu, utataka kuwaambia watu wengine kuhusu Yesu. Unaweza kuwa shahidi – mtu anayewaambia wengine kile Mungu amewafanyia.

Katika Marko 5:19 Yesu alisema, “Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu.” Sote tuna marafiki, majirani na jamaa ambao hawamjui Yesu kama Mwokozi wao kibinafsi. Hakikisha unawashirikisha yale ambayo Yesu amekutendea.

Hapa kuna mambo machache ambayo lazima uyajue kabla ya kuongea na mtu kuhusu Yesu:

1. Jua ya kuwa wewe ni Mkristo. (Yohana 5:24)
2. Jua ya kuwa Mungu anampenda kila mtu. (Yohana 3:16)
3. Jua ya kuwa kila mtu ametenda dhambi. (Warumi 3:23)
4. Jua ya kuwa kila mtu lazima aungame dhambi zake kwa Yesu. (1 Yohana 1:9)
5. Jua ya kuwa Mungu aliahidi uzima wa milele kwa wale walio mwamini. (Warumi 6:23)
6. Jua ya kuwa Yesu yuko tayari kumpokea kila mtu anayeomba. (Mathayo 21:22)

Wakati rafiki yako au jamaa yeyote anapokiri dhambi zao kwa Yesu na kumwomba msamaha, wanakuwa washirika wa familia ya Mungu kama wewe. Kumbuka, Yesu alikufa kwa ajili ya kila mtu katika ulimwengu wote.

*Shirikisha marafiki zako wapya wa Kikristo umuhimu wa-*

1. Kusoma Biblia zao kila siku.
2. Kuzungumza na Mungu kila siku.
3. Kuhudhuria shule ya Jumapili na kanisa wakati wote.
4. Kuwaambia wengine kuhusu Yesu.
5. Kuishi maisha ya Kikristo mbele za wengine.

Kuna njia nyingi za kuwaambia wengine kuhusu Yesu. Hapa ni mapendekezo macahache. Jaribu!

**WAAMBIE WENGINE KWA—**

1. Kutumia sauti yako. Uwaambie kile Yesu amekufanyia.
2. Wapatie trakti za hadithi zinazozungumza habari za Yesu.
3. Kuishi maisha ya Kikristo.
4. Kuwaalika waende kanisani pamoja nawe.
5. Kuwaandika barua au maelezo na kuwashirikisha.



Yesu anataka tuwaambie wengine juu yake. Je! Anaweza kukuhesabu kuwa kama shahidi wake?

Ndiyo, Yesu anaweza kunitegemea \_\_\_\_\_  
kuwa shahidi kwake. (andika jina lako hapa)

## ULIJIFUNZA NINI KUTOKA KWA KUSOMA KWAKO?

1. Je! Tunapata wapi mistari kwenye Biblia ambayo yanatuambia kwamba tunapaswa kwenda kuwaambia wengine habari za Yesu?

\_\_\_\_\_

2. Jibu maswali yafuatayo kwa "Ndiyo" au "Hapana."

- A. Kila mtu ametenda dhambi. \_\_\_\_\_  
B. Mungu anapenda Wakristo tu. \_\_\_\_\_  
C. Kila mtu lazima azikiri dhambi zake. \_\_\_\_\_  
D. Yesu atatusamehe kila wakati. \_\_\_\_\_

3. Nini unapaswa kumwambia Mkristo mpya afanye? Weka X kwenye kila sentensi ambayo ni sahihi.

- \_\_\_\_\_ Omba Jumapili tu.  
\_\_\_\_\_ Soma Biblia kila siku.  
\_\_\_\_\_ Hudhuria kanisa Jumapili tu.  
\_\_\_\_\_ Waambie wengine kuhusu Yesu.  
\_\_\_\_\_ Ishi maisha ya Kikristo mbele za ya wengine.

4. Orodhesha njia mbili ambazo tunaweza kuwaambia wengine kuhusu Yesu.

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

5. Kwa nini tunapaswa kuwaambia wengine kuhusu Yesu?

\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_



6. Tengeneza orodha ya watu watatu ambao utaweza kuwaambia habari za Yesu.

---

---

---

7. Orodhesha vitu vitatu unavyopaswa kujua kabla hujamwambia mtu mwingine kuhusu Yesu?

JUA \_\_\_\_\_

JUA \_\_\_\_\_

JUA \_\_\_\_\_

8. Orodhesha mistari ya Biblia (kitabu, sura, mstari) ambayo itakusaidia katika kuwaambia wengine.



---

---

---

---

---

---



9. Tathmini mistari ya Biblia ambayo tayari umejifunza moyoni mwako.

10. Kukariri mstari huu wa Biblia-

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi." (Yohana 14:6)

Hii ni orodha ya mistari muhimu ya Biblia katika kozi hii ambayo unahitajika kujifunza moyoni mwako.

Luka 2:52

Mathayo 24:35

Yohana 3:26

1 Yohana 1:9

Marko 11:24

Mathayo 6:9-13

Unapomaliza kijtabu hiki, peleka kwa mwalimu wako ambaye atakiangalia zaidi, ataangalia karatasi zako za kazi na atakurudishia.







**FMP**

Foursquare Missions Press

Living the Christian Life - Swahili  
Foursquare Missions Press © 2003  
pamoja na *Mizizi* Mobile Missions © 2020